(vi) Aje na kiatu cha wazi (open shoes) nyeusi yenye mikanda nyeusi na iwe na mkanda unaofunga kwa nyuma.
(vii) Mkanda mweusi wa ngozi
(viii) Aje na Ream Mbili ( A4) ( NB:Aje na vifaa na siyo fedha) .
(ix) T-shirt ya bluu yenye shingo ya kola yenye nembo ya shule ambayo atavaa siku ya jumatano na ijumaa tu (INAPATIKANA KWENYE DUKA LILILOPO SHULENI KWA BEI YA SH 15,000/=).
(x)Tai mbili za rangi ya nyeusi ikiwa na nembo ya shule (HII INAPATIKANA KATIKA DUKA LILILOPO SHULENI KWA BEI YA SH 5000/=).

**(B)SARE YA KAZI ZA NJE**

(i)Baada ya masomo ( wakati wa kazi za nje na kushindia) sare inayovaliwa ni suruali nyeusi na T-Shirt ya bluu.
(ii)Aje na raba kwa ajili ya michezo iwe rangi nyeusi yenye kamba, sole ya kawaida na sio mfano wa buti (boot) NB:Usije na nguo za nyumbani wala redio, simu, au laini ya simu
(iii)Track-suit ya rangi ya bluu yenye michirizi/mistari myeupe pembeni ya miguu na mikononi na isiwe na nembo ya club yeyote ya mpira ila yaweza kuwa na nembo ya kampuni iliyoitengeneza
(iv) T-shirt ya bluu yenye shingo ya duara yenye nembo ya shule (HII INAPATIKANA KWENYE DUKA LILILOPO SHULENI KWA BEI YA SH 10,000/=).

**(C)SARE YA MICHEZO**

Shule inasisitiza michezo kwa afya na makuzi bora.Hivyo aje na vifaa vifuatavyo kwa ajili hiyo:
(i)Bukta mbili rangi ya bluu zenye michirizi miwili pande zote.
(ii)Viatu vya raba vyeusi vyenye kamba kwa ajili ya michezo.
**NB**: T-shirt ya rangi ya bluu yenye shingo ya duara iliyotajwa hapo juu ndiyo itatumika kama t-shirt ya michezo na kushindia lakini ni muhimu kuzingatia usafi.

**(D)MALAZI**

Shule inatoa kitanda tu hivyo uje na:
(i) Godoro dogo(lenye viwango na ubora)la“Sponge”lenye ukubwa wa 6’x2½‘x 4’na lenye“cover”.
(ii) Shuka mbili rangi ya Pink iliyokolea,mto na foronya mbili za Pink
(iii) Kandambili jozi moja kwa ajili ya kuogea.
(iv) Uje na mswaki,dawa ya mswaki ,sabuni za kufulia na kuogea za kutosha muhula mzima
(v) Uje na chandarua ya bluu kwa ajili ya mbu
(vi) Uje na toilet paper kwa matumizi yako.

## 2.2 VIFAA VYA KULIA CHAKULA

Shule haina utaratibu wa kugawa vyombo vya kulia,hivyo uje na sahani ,bakuli , kikombe na kijiko kwa ajili ya kuchukulia chakula na kulia.

## 2.3 VIFAA VYA USAFI

Uje na fagio la ndani ( soft broom) ,reki na mpini ,Fyekeo,fagio la nje( chelewa) ,sqeezer, fagio la kusafishia choo( hard broom) ,Jembe na mpini wake na ndoo ndogo mbili kwa ajili ya usafi wa maeneo anayoishi hapa shuleni( NB:Uje na vifaa na siyo fedha).

